# EPISODE 4 “PLAY AND PAY!”

**SCRIPT WRITER** **Njoki Muhoho**

**EDITOR** **Jan-Philipp Scholz**

**KISUAHELI** **Eric Ponda**

**CHARACTERS**

| | |
|---|---|
| **ANNOUNCER** | Male Adult |
| **ZAPCOM** | A 23-year-old computer geek, by village standards. |
| **GEORGE** | 20 years old. Waits tables at his Uncle Kilu’s restaurant. |
| **AUNTI BONGI** | 38-year-old ICT Manager in the big city and Zapcom’s favourite Auntie |
| **CUSTOMER** | Mid 20’s |
| **UNCLE KILU** | 55 years old. George’s uncle, owner of KULA TU FOODS. |
| **OMWA** | 19 years old and jobless. Female. |

**INTRO**

1. **MUSIC: THEME MUSIC**

2. **ANNOUNCER** HUJAMBO MPENZI MSIKALIZAJI WA DEUTSCHE WELLE MAHALI POPOTE ULIPO NA KARIBU KWA MAKALA YETU YA NNE YA MFULULIZO WA MCHEZO WA REDIO

"LEARNING BY EAR", 'NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO'. BADO TUKO KATIKA MASUALA YA TEKNOLOJIA MPYA YA HABARI NA MAWASILIANO KATIKA MCHEZO HUU WA LEO KWA JINA KUCHEZA NA KULIPA YAANI '***PLAY AND PAY'***

KATIKA KIPINDI KILICHOTANGULIA , BAADA YA ZAPCOM KUZINDUA HUDUMA ZA MTANDAO WA INTANETI KIJIJINI MWAKE, BIASHARA YAO SASA IMEIMARIKA HARAKA KULIKO ILIVYOTARAJIWA.PIA WAMEWEZA KUWASHAWISHI WATEJA WAO KUTUMIA SIMU ZAO ZA MKONONI KUUNGANISHWA NA MTANDAO WA INTANETI. HATIMAYE GE0RGE ANAANZISHA BIASHARA YA KUUZA KADI ZA SIMU AMBAYO INAMLETEA FAIDA. HATA HIVYO KUNDI ZIMA SASA LIMEANZA KUKABILIWA NA CHANGAMOTO ZINAZOAMBATANA NA HUDUMA HIZI MPYA HASA KATIKA MAZINGIRA YA KIJIJI AMBACHO MUUNDO MISINGI YAKE NI DUNI. JE BIASHARA YAO ITAFAULU KATIKA MAZINGIRA HAYA. ENEDELEA KUTUSIKILIZA.

**SCENE 1: KULA TU FOODS**

**3. A-SFX: SHUFFLE OF FEET AS UNCLE KILU WALKS AROUND THE RESTAURANT PANTING**

**4. UNCLE KILU** (**MUTTERING TO HIMSELF**)
Haiwezekani…inatumika ...hakuna… inatumiwa … (VERY ANGRY) aaaaggggghhh. Siwezi hata kupata plagi yoyote hapa kazini?

**5. ZAPCOM** **(CONCERNED)** Mzee, kuna nini ?, una shida gani?

**6. UNCLE KILU** (**ANGRY**) Nitawezaje kuwa sawa ikiwa siwezi hata kusikiliza stesheni yangu niipendayo

**7. ZAPCOM** Kwa nini usiweze kusikiliza Mzee? Una haki ya kufanya hivyo, hapa ni kwako Mzee!

**8. UNCLE KILU** (**MORE ANGRY**). Hilo ndilo tatizo. Siwezi kuwa nazunguka huku na huko hapa mkahawani na redio yangu mkononi nikionekana mgeni kama kuku aliyenyeshewa, radio yangu inapasa kuwa imeunganishwa kwa plagi ya stima mahali pamoja. (**PAUSE**) Redio stima…stima …..Redio…. Unaelewa Zapu?

**9. ZAPCOM** (CALM) Kumbe sasa naelewa shida yako

10. **UNCLE KILU** **(GETTING BALLISTIC)** Mimi…? Eti nina shida? Hapana Zapu sina shida, sina shida, wewe ndie mwenye shida… wewe na hawa vijana wote walio hapa. Mnatumia plagi zote za stima katika mkahawa huu. Angalia… hebu angalia watu wote hapa kijijini wanakuja kutumia stima yangu kuchaji simu zao hapa kwa nini …kwa nini wanafanya hivyo?

11. **ZAPCOM** Eeeh. Kwa sababu… kwa sababu eee

12. **UNCLE KILU** (**INTERRUPTS**) Ndio … kwa sababu yako Zapu…..! wewe na hizi komputa zako nyingi nyingi tu, na sasa kila mmoja hapa kijijni anakuja hapa na simu yake ya mkononi, waya masikioni na mwengine kwenye plagi za stima. Kwanza umeona bili ya stima hivi karibuni.?

13. **B-SFX: DOOR OPENS WITH A BANG AND SHOPPING BAG PAPERS SHUFFLE**

14. **OMWA** Hamjamboni nyote…_? mnajua nimemuletea nini………

15. **(MORE SHUFFLING OF PLASTIC SHOPPING BAGS)**

| | | |
|---|---|---|
| **16.** | **OMWA** | (VERY EXCITED) Kiunganisho cha stima! Unaona… unaona.. kila plagi hapa inatumika, kwa hivyo tukiongeza kiunganishi kingine cha stima kila mmoja wetu atapata nafasi ya kutumia stima kuchaji simu yake …. |
| **17.** | **UNCLE KILU** | (**EXASPERATED**)…OMWA… usifanye….. usifanye hivyo! |
| **18.** | **ZAPCOM** | Omwa subiri kwanza, subiri…! |
| **19.** | **C-SFX: BIG BANG AS THE POWER SWITCH TRIPS** | |
| **20.** | **(SILENCE)** | |
| **21.** | **UNCLE KILU** | (CONTROLLED CALMNESS-STILL WITH ANGER) Kisha, ni giza sasa ! |
| **22.** | **ZAPCOM** | Amen. **(PAUSE**) Omwa? |
| **23.** | **OMWA** | (**SCARED**) Zap. |
| **24.** | **ZAPCOM** | Sasa tumejikaanga na mafuta yetu! |

**25. ANNOUNCER** Kila lililo jema halikosi kasoro, hali kadhalika maendeleo huja na changamoto zake pia. Sasa wanafurahia teknolojia mpya ya simu za mkononi lakini kuna masuala yanayojitokeza kuwa changamoto kubwa kama vile kuchaji simu kila mara. Si jambo geni kwa Bara la Afrika kukumbwa na changamoto za aina hii hasa tunapozungumzia suala la kiteknolojia na hivyo hakuna sababu yoyote ya kukata tama na kupuuzilia mbali teknolojia hii mpya ya mawasiliano au zaidi mradi ulioanzishwa na George na Zapcom. Wao pamoja na wateja wao lazima wang'ng'ane kusonga mbele. Lakini kwanza lazima wamshawishi Mjomba Kilu ambaye amewaita tena ofisni mwake kwa mazungumzo ya faragha

**MUSIC: BRIDGE MUSIC**

**SCENE TWO: BACK OFFICE OF KULA TU FOODS, SILENCE**

**26. D-SFX: HEAVY BREATHING.**

**27. ZAPCOM** Pole sana Mzee!

**28. GEORGE** Hatukujua mwishowe hali itatokea hivi…….

**29.** **UNCLE KILU** Kwa kweli hamna habari ni kwa kiwango gani munavyoathiri biashara yangu….! Dhamira yangu katika biashara hii ni kuwauzia wateja wangu chakula kizuri kila siku na haijatokeo hata siku moja kwa akili yangu kwamba ningetoa huduma za stima kwa zaidi ya watu 20 wanaovamia mgahawa wangu kuchaji simu zao.

**30.** **GEORGE** Lakini mjomba si wote walio na stima majumbani mwao na bado wanataka kutumia simu zao kila wakati mahali popote.

**31.** **UNCLE KILU** (**RUNNING OUT OF PATIENCE**) Sasa kwa nini….. heee…. kwani mtu ananue teknolojia mpya na hana uwezo wa kudumisha?

**32.** **ZAPCOM** (**IN HIS TEACHER MODE**) Kama ujuavyo sisi hapa barani Afrika hatuna zile huduma zinazotajwa na mataifa yaliyostawi kuwa huduma za kimsingi. Lakini haina maana kwamba tuendelee kubakia nyuma kwa sababu ya ukosefu wa huduma hizo. Ni lazima tujikakamue kusonga mbele na wakati. Hatuwezi kuwaambia watu wetu wasinunue simu za mkononi kwa sababu ya ukosefu wa stima nyumbani kwao kuchaji simu!.

**33.** **UNCLE KILU** Usemavyo ni sawa kabisa, lakini …. Lakini

**34. GEORGE** Sawa basi mjomba, tutachanga kulipa bili ya stima na gharama nyinginezo ndogo ndogo!

**35. UNCLE KILU** Hilo sio suala tunalozungumzia hapa! Tatizo ni kwamba siwezi tena kuendesha shughuli zangu za kawaida kwa sababu plagi zote zinatumika, na sasa hata fyuzi zote zinalipuka mara kwa mara.. Hamuoni tunakumbwa na tisho?.. moto unaweza kutokea wakati wowote!

**36. ZAPCOM** Hebu tumutafute fundi wa umeme mara moja aje akague mahali hapa..

**37. UNCLE KILU** Na hiyo ni kumaanisha gharama zaidi,…kwani mimi pia nahitaji plagi yangu pekee yangu nitumie kwa redio hii yangu iliyochakaa!

**38. ZAPCOM/GEORGE** Sawa tumekubaliana!.

**39. GEORGE** Lakini unaweza kuendelea kusikiliza vipindi vya redio kupitia simu yangu ya mkononi….. shika ..tumia hiki chombo cha kusikilizia (**RUSTLE OF CLOTHES**)

**40. E-SFX: STIFLED. ZAPCOM AND GEORGE TRY TO SURPRESS LAUGHER AS UNCLE KILU MOVES AWAY HUMMING TO MUSIC FROM THE MOBILE PHONE RADIO**

**41. ANNOUNCER** Yote yanategemea mtazamo wako na namna unavyoweza kukabiliana na changa moto maishani.Na ndivyo vijana hawa wanavyojifunza kukabiliana na changamoto hizo. Kuendesha biashara ya huduma za Intaneti si jambo rahisi kama walivyodhania.. Lakini je matatizo yao yanaishia hapo? Kutokana na kupanuka kwa biashara yao, Zapcom na George wameamua kumuajiri Omwa ili awasaidie kazi ya usimamizi katika mkahawa wao.Lakini ujuzi wake wa Komputa bado unayumba sana, ingawa anaweza kuwasaidia wateja kufungua na kufunga Komputa mbali na kuchukua malipo ya huduma hizo.

**SCENE THREE: BACK OFFICE KULA TU FOODS**

**42. E-SFX: HEAVY ANGRY FEET STRODDING IN**

**43. ZAPCOM** (**ANGRY AND LOUD**) OMWA! Kwanini huchukui simu?Tumekuajiri katika ofisi hii kufanya kazi zote za uimamizi, ikiwa ni pamoja na kujibu simu!. Hatuwezi kukulipa mshahara ikiwa huwezi kufanya kazi yako ipasavyo.Na hii ni pamoja na kujibu simu tunapokuwa nje ya ofisi. .

**44. OMWA** Lakini ni kwa…. ni kwasababu sina pesa!

**45. ZAPCOM** … Bila kufanya kazi huwezi kulipwa mshahara, na hiyo ni kusema huna kazi. Ni mara ngapi utaachishwa kazi ndani ya muda wa mwezi mmoja!

**46. GEORGE** Pole pole Zap, pole pole , usiwe mkali kwa msichana

**47. OMWA** Sikuwa na pesa kwa simu yangu

**48. ZAPCOM** Oh?

**49. OMWA** Nilitaka sana kuzungumza nanyi kwa simu na hata marafiki wangu wote, lakini nitafanyaje ikiwa sina pesa za kunua kadi ya simu..?

**50. ZAPCOM** Sio wewe pia. Mjomba Kilu anasema hakuna haja ya kuwa na simu ya mkononi iwapo hatuwezi kuzichaji nyumbani! Una simu na huna pesa za kunua kadi. Kwa nini?, Kwa nini wasiweke matangazo ya biashara, kama vile kadi bora na za bei nafuu, na kadhalika, Siku yangu imeanza vibaya.

**51. CUSTOMER** (**SHOUTING LOUDLY**) Wewe, mimi sitailipia

**52. ZAPCOM** (**FRUSTRATED AND MUTTERING**) Sasa ni nini (**LOUDLY**) … Kuna shida gani?

**53. CUSTOMER** (**ANGRY**) Hebu tazama, tazama hii skrini ya Komputa

**54. ZAPCOM** (**BUFFLED)** Ehhh ina nini?… sioni kitu mimi…giza tu!

**55. CUSTOMER** (**WITH GLEE**) Unaona …. hakuna kitu…. Nimesubiri hapa kwa zaidi ya muda wa dakika kumi hivi na hii komputa haifunguki.. (**GETTING ANGRIER**), Kwa nini inafunguka pope pole. Mimi natumia pesa nyingi na huku sipati huduma ninazohitaji. Bwana…kasi ya Komputa yako ni ya pole pole sana kushinda mwendo wa kobe barani Afrika..

**56. OMWA** (**MEEKLY**) La hasha si kama kobe!

**57. CUSTOMER** Basi tuseme mwendo wa kono kono !Kusema kweli mimi siwezi kukulipa..!

**58. F: SFX: CRUSHING SOUND AS HE PULLS CHAIR ROUGLY AND WALKS OUT.**

**59. ZAPCOM** (**SOFTLY**) Kwa nini iwe hivi lakini

**60. ANNOUNCER** Kama kuna siku Zapcom amekumbwa na changamoto katika teknolojia mpya ya mawasiliano barani Afrika, bila shaka ni siku ya leo. Lakini bado ana chaguo. Aidha asubiri kwa matumaini kwamba huduma hizo zitaimarika na kuwa kama zinazopatikana katika mataifa yaliyostawi au kujitahidi na kile alichonacho. Kwa Zapcom maisha yemembadilikia ghafla na kuanza kujiona mpweke.

**61. G-SFX DIALING OF A PHONE**

**62. AUNTIE BONGI (VO)** (**EXCITED**) Zapcom, binamu yangu, sijakusikia ukiongea kwa muda sasa. Je unaendeleaje na biashara yako? …Mimi…

**63. ZAPCOM** (**VERY LOW**) Shangazi naendelea vizuri. Lakini nahitaji ushauri wako..!

**64. H-SFX: LOW BATTERY PEEP**

**65. AUNTIE BONGI (VO)** Kwani umepatwa na matatizo. Unaonekana mnyonge na mwenye shida nyingi. Una shida gani?

**66. ZAPCOM** Kwa kweli najihisi mnyonge sana, siku yangu ilikuwa mbaya sana, huduma zetu za mtandao wa Intaneti zimekuwa za pole pole sana (**BATTERY BEEP**), na hata simu yangu imeisha moto. Hatukuwa na umeme karibu siku nzima baada ya kutokea matatizo kazini. Mbali na hayo nataka kwenda …

**67. ZAPCOM** (**SADLY**) Ooh sasa, betri yangu ya simu imeisha moto kabisa!

**68. OMWA** (**MEEKLY**) Zapcom, Unaweza …..Unaweza kunipa rubuni ?

**69. I-SFX: HEAVY SHUFFLE OF FEET**

**70. UNCLE KILU** Zapu, unaonekana mwenye majonzi sana. Kesho pia ni siku. Mambo huenda yatabadilika.

**71. ZAPCOM** Una hakika? Huu ndio wakati ninapohitaji sana ile supu ya mbuzi. Itaweza kunichangamsha japo kidogo.

**72. UNCLE KILU** **(HESITANT)** Pole sana Zapu… leo hatukuwa na nyama ya mbuzi….. kwa hivyo eehhh pole sana .

**MUSIC: BRIDGE MUSIC**

**ANNOUNCER** Ama kwa hakika imekuwa siku mbaya kwa ZAPCOM. Lakini je ataweza kuimudu hali hii au atazama katika wimbi la unyonge. Licha ya kufanya kila awezalo, bado shida zinaendelea kumuandama !

**73. MUSIC: THEME MUSIC**

**OUTRO**

74. **ANNOUNCER** Hii ni sawa na kuweka kileo kipya kwa chupa za zamani!. Ingawa Zapu amekuja na wazo zuri la teknolojia mpya ya mawasiliano, je atafaulu hasa katika sehemu za mashambani Barani Africa. Au wazo hili atalitupilia mbali? Je Mjomba Kilu baada ya shida alizopitia atakubali kuendelea kuwa mshirika wa kibiashara na kundi hili la vijana. Kwa hakika teknolojia hii ya mawasiliano ya kissa ni kama mkondo wa Mto. Na ukiyavulia nguo basi huna budi ila kuyaoga. Lakini Je Zapcom na kampuni yake itanusurika katika dhoruba hili.

Ungana nasi kwa makala ijayo usikie mambo yatakavyokwenda. Ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki au kupata

maelezo zaidi kuhusu vipindi vya "Learning By Ear" Noa Bongo jenga maisha yako tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe . Na ukiwa na maoni usisite kututumia, na itakuwa furaha yetu kuyapokea.Na kufikia hapo hatuna buddi ila kufunga virago studioni hadi wakati mwengine Kwaheri kwa sasa.